

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa  
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## MUNGU NI KIMBILIO LETU

*Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. —Zaburi 46:1.*

Je, ni kwa nini ni muhimu kwetu kuwa na mahali pa kukimbilia? Je, ni kweli kwamba wokovu ambao tunapata kupitia kwa Yesu Kristo hukinga watoto wa Mungu dhidi ya shida za kidunia, maumivu, na majonzi maishani haya? Jibu rahisi kwa swali hilo ni “la, hasha.” Wokovu ni ujuzi spesheli ambapo mtu hupata kuokoelewa kutokana na dhambi na hukumu. Mwokovu huyo anapata amani ya ndani, furaha ya Roho Mtakatifu, na tumaini la uhai wa milele. Lakini kwa sababu yeye angali anaishi katika ulimwengu uliojaa dhambi, na angali kiumbe ambacho kina hisia za aina tofauti tofauti, basi hana budi kukutana na mambo magumu ya maisha haya. Kuna siku ambapo jua halitachomoza, na majonzi ya nje na ndani maishani mwetu yatajaribu kuandama nafsi zetu. Roho ya mwanadamu ikiandamwa na mambo magumu, huo ndio wakati ambapo anahitaji kuwa na mahali pa kimbilio maishani.

Tunamshukuru Mungu kwa sababu kuna kimbilio ambalo tunaweza kutorokea wakati wa shida. Zaburi 46 ni andiko la maliwazo ambalo linahudumia mioyo ambayo inauma, na nafsi ambazo ziko katika hatari ya kuzama kutokana na masumbuko ya maisha. Neno kimbilio linaashiria mahali pa kujikinga, mahali penye matumaini, mahali pa kutorokea, ili kupata usalama. Hata ingawa kila mtu duniani ana shida zake, watu wengi hutafuta maliwazo na faraja katika mambo ya kidunia. Lakini hakuna kitu ambacho kinaweza kulinganishwa na kimbilio ambalo hupatikana ndani yake Mungu. Kwa kweli Yeye atatupatia mahali pa usalama na faraja, na pia atatuhudumia na kutuliwaza dhidi ya uchungu ambao wengi wetu wanapitia katika siku hizi tunazoishi.

Watu wengi wa Mungu wanapitia nyakati ambazo zina giza nyingi; wengine wao wamefungia shida hizo mioyoni mwao na kuzifunika kwa tabasamu sisizo za kweli usoni mwao; lakini bado uchungu na majonzi yao yangali yawauma ndani kabisa katika roho zao. Basi wewe mtoto wa Mungu, kuna msaada ambao unaweza kupata kwa moyo wako ambao unauma. Mungu anakusubiri umkimbilie na roho hiyo yako iliyovunjika, na Yeye atakukumbatia kwa mikono yake ambayo imejaa faraja, upendo, na kukujali. Yeye ni “msaada wa karibu wakati wa shida.” Yeye kamwe hatachelewa, na atakuwa hapo karibu nawe ili akusaidie na kukupatia msaada wa kukufaidi kwa swala lolote lile ambalo linakuletea wasiwasi, masumbufu, na hata majonzi.

Nabii Isaya aliandika ukweli kuhusu usalama na hifadhi ambayo Mungu huwapa watu wake: “Maana umekuwa ngome ya maskini, ngome ya mhitaji katika dhiki yake, mahali pa kukimbilia wakati wa tufani, kivuli wakati wa hari” (Isaya 25:4). Katikati mwa mawimbi ya maisha haya ambayo sasa yanavuma kwa nguvu, na ambayo yanajaribu kushinda nafsi zetu, tuna hifadhi katika Mwokozi wetu. Wewe mtoto uliyechoka, hebu jua kwamba huko peke yako. Yesu Kristo anakutazama kwa moyo wa huruma ili akusaidie dhidi ya misukumo ambayo inakukabili sasa, na Yeye ameahidi kwamba atakuwa nawe. Isaya 43:1-3 inasema: “Lakini sasa, BWANA aliyekuhuluku, ee Yakobo, yeye aliyekuumba, ee Israeli, asema hivi, usiogope, maana nimekukombo; nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu. Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza. Maana mimi ni BWANA, Mungu wako;

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



**“Wewe mtoto uliyechoka, hebu jua kwamba huko peke yako. Yesu Kristo anakutazama kwa moyo wa huruma ili akusaidie dhidi ya misukumano ambayo inakukabili sasa, na Yeye ameahidi kwamba atakuwa nawe.”**

Taharir  
3

Ahadi Za Mungu  
4-5

Wakati Wa Shida  
5  
Funga Mlango Wa  
Moyo Wako Kwa  
Shaka  
6

Kutazama Jua  
Lichomoza  
Kuimba Wakati Wa  
Shida  
6

Imani yako iongoze  
hisia  
Kutokana Na  
Kushindwa Tupate  
Ushindi  
7

Je, Wajua?  
Mateso Humwezesha  
Mtu Kuwa Na Huruma  
Na Watu Wale Wengine  
8

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

## Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

## Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

## Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

## Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

## Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

## Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

## Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

## Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

## Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

## Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

## Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

## Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

## Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

## Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

## Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

## Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

## Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

## Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

Mtakatifu wa Israeli, mwokozi wako.” Ahadi ya Bwana haisemi kwamba hatutapitia katika mito na moto, bali inatuahidi kwamba mambo haya hayatatulemea, na kwamba Yeye atakuwa pamoja nasi tunapoyapitia.

Kwa maana Mungu ni kimbilio letu na nguvu zetu Daudi akasema, “Kwa hiyo hatutaogopa . . .” Hata ingawa tutakumbwa na shida za kiroho, za kisiasa, za kifedha, na hata zile zinazohusiana na uhusiano na wanadamu wenzetu, hatuna haja ya kuogopa, kwa sababu Mungu yumo katikati mwetu, na Yeye atawasaidia watu wake. Zaburi 46:5 inasema “Mungu atakusaidia asubuhi na mapema.” Hata tafsiri nyingine inatumia maneno ya kuvutia zaidi inaposema

“Hebu pumzisha roho yako  
ambayo imechoka ndani  
ya mikono mwake Yesu  
Kristo ambayo ina nguvu,  
na Yeye atakushikilia na  
kukuinua unapotembea  
jangwani hilo ambalo  
unapitia kwa sasa.”

kwamba “jua lichomozapo.” Hata wakati wa usiku uliojaa giza Mungu atatupatia msaada na kutuletea jua la asubuhi. Ndani mwake Yesu Kristo mna tumaini kwa wale ambao wamepoteza tumaini, hata waliotahayarika wanaweza kupata ujasiri, na waliovunjika mioyo wakapata uponyaji.

Ni masaa ya usiku wa manane ambako kunaonekana hakuna mwisho wa matatizo yanayotukabili ndipo miali ya mwangaza inapenyeza na kuangaza humo gizani. Basi kama wewe uko

vitani, mahali ambako kuna msukumano mkubwa, hebu usikate tamaa. Hebu pumzisha roho yako ambayo imechoka ndani ya mikono mwake Yesu Kristo ambayo ina nguvu, na Yeye atakushikilia na kukuinua unapotembea jangwani hilo ambalo unapitia kwa sasa. Kama utamtumaini Bwana, Yeye atabadilisha jangwa lako na kulifanya kuwa kisima cha maji, na usiku wenye giza utabadilika na kuwa mchana wenye kujaa mwangaza.

Ni wakati ambapo akili zetu zimechanganyikiwa, na roho zetu zikawa hazioni njia ya kuepuka shida zinazotukabili, ndipo Bwana anatwambia, “Acheni, mjue ya kuwa mimi ni Mungu” (Zaburi 46:10). Mambo yote yanawezekana ndani yake Mungu, na kamwe Yeye hatawaacha wale ambao wanamtumaini.

Uzima tele ni ujuzi ulio wa kweli ambao unapatikana wakati mtu anaishi kama Mkristo, lakini hii si kumaanisha kwamba sisi tutaepuka vita vya ndani na nje wakati tunapoishi ulimwenguni huu ambao una masumbufu yake. Lakini habari njema ni kwamba, sisi tunalo kimbilio ambalo tunaweza kukimbilia, “Lakini twajikosesha, twajitweka vibaya; kwamba tulimwomba Mungu dua angesiki” (Yesu Kwetu ni Rafiki/What a Friend we have in Jesus). – Ndugu Michael Smith

UNAWEZA KUPATA VITABU VILIVYOTAJWA KATIKA TOLEO HILI KUTOKA KWA TOVUTI YA:

[www.churchofgodeveninglight.org](http://www.churchofgodeveninglight.org)

MIALI YA TUMAINI

SIRI ZA MOYO ULIO NA WIMBO

MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya [www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org) na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA  
[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

# Tahariri



*Nikaapo gizani, BWANA atakuwa nuru kwangu. —Mika 7:8*

Yesu alikuja ulimwenguni kutokana na upendo mkuu wa Baba yake. Ndiposa akapitia machungu, majonzi, na mateso ya wanadamu ili aweze kutuombea kwa huruma na kwa kutuelewa. Katika wakati ambapo mmejaa giza la kiroho, Yesu alikuja ili awainue wale ambao walikuwa wameanguka, na kwa ajili ya kuleta mwangaza katika nafsi zilizojaa giza.

Lakini hata baada ya kupata ukombozi na kutoka dhambini kwa njia ya neema na wokovu unaopatikana ndani ya Bwana wetu Yesu Kristo, mwanadamu hana budi kupitia vitani na majaribu ya ulimwengu huu. Adui wa nafsi yako anafanya juu chini ili kudidimisha tumaini lako na kukuletea hali ya kukata tamaa. Lakini kwa nguvu zote ambazo tuko nazo, tunahitaji kushikilia ahadi zake Mungu, na pia kushikilia msalaba, kwa sababu hapo ndipo kunapatikana mwangaza na uhai.

Somo la robo hii ya mwaka linahusu “Wakati wa Shida.” Hata ingawa lengo langu sio kumpatia adui yetu Shetani heshima wala kutilia shaka amani ya ajabu ambayo inapatikana ndani yake Bwana Yesu; kwa njia ya wazi kabisa sisi tunasema kwamba bado kuna matatizo yanayotandama maishani mwetu hata baada ya mtu kuokoka. Kamwe hatukombolewi kutokana na masumbufu ya ulimwengu huu hadi wakati tutakapoingia Mbinguni, ambako ndiko nyumbani mwetu milele. Lakini ni baraka kuu kwamba kuna Bwana ambaye anatembea nasi ‘sako kwa bako’ na kutusaidia wakati wa shida.

Sisi tunahubiri ujumbe wa ushindi na kuishi kulingana na ushindi huo kwa neema yake Mungu. Lakini kuna wengi wetu ambao wamejipata wako karibu kushindwa kabisa, na giza la kukata tamaa na misukumo inayotoka ndani na nje, wakawa wanabeba mizigo mizito sana. Mimi kamwe sitaki kupunguza uzito wa ukweli kwamba kuna mashindano ambayo watu waliookoka wanaweza kuwa nayo rohoni mwao, katika hisia zao, na hata kwa jinsi wanavyojisikia n.k. wakati ambapo wanafanya safari ya kumwishia Mungu hapa ulimwenguni.

Toleo hili ni tofauti na toleo zile zingine kwa sababu hapa nitashiriki maandishi ya toleo za awali, ambayo ni maombi yangu kwamba yatakuwa baraka na kuleta faraja kwa watu wanaopitia katika nyakati za shida. Hata mimi mwenyewe nishawahi kukaa gizani zaidi ya mara moja maishani mwangu ya Kikristo na nikagundua kwamba ni ule uwepo wa upendo wa Mungu, na kutambua jinsi anavyonijali, ndio mambo ambayo yaliniletea uponyaji katika akili na rohoni mwangu. Ukweli ni kwamba, Mungu ni kimbilio ambalo halina tashwishi, na ndio sababu tunahitaji kudumu katika sitiri ya upendo wake katika siku ambazo tunaishi, hata zaidi ya vile tulifanya katika siku za hapa awali.

Watoto wetu na vijana wetu wanapitia misukumo na mashindano ambayo vizazi vya mbeleni hawakupitia. Adui yetu habangui, na anawavamia watakatifu kwa hasira. Lakini nguvu za Mungu ni zaidi ya nguvu za adui, na ni mwangaza wa Mungu tu ndio utafanya giza kuondoka. Wakati mwingi watu walio-okoka huona aibu kukubali mashindano yao ya kindani, na wakati mwingi wao pia hawapati mahali muafaka ambako hali halisi ya vita ambavyo vinawakabili inaweza kujadiliwa kwa uwazi. Lakini Mungu ndiye mwenye jawabu la mwisho na Yeye atakuwa “ngome yao wakati wa taabu” (Zaburi 37:39). Hii ndio sababu mimi ninatoa himizo kwamba yeyote ambaye anaumia basi amtafute mtu ambaye ataweza kuwa mwandani na msiri wake, ili waweze kuzungumza na kuomba pamoja ana kwa ana, na ili nguvu za giza ziweze kuvunjiliwa mbali.

Basi hebu jua kwamba unapendwa, kwamba hauko peke yako, na kwamba Mungu atakuwa mwaminifu kwako!

Michael W. Smith

Aprili 2021.

“HUENDA KILIO HUJA KUKAA USIKU,  
LAKINI ASUBUHI HUWA FURAHA”  
ZABURI 30:5



Tutembelee

[www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org)

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.

# Ahadi Za Mungu

*Mradi atanisitiri bandani mwake siku ya mabaya, atanisitiri katika sitara ya hema yake, na kuniinua juu ya mwamba. —Zaburi 27:5*

## MUNGU ANAKUPENDA

BWANA alinitokea zamani, akisema, naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu. —Yeremiah 31:3



Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? . . . Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye

mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu. —Warumi 8:35-39

## MUNGU NI MWENYE HURUMA

Ni huruma za BWANA kwamba hatuangamii, kwa kuwa rehema zake hazikomi. Ni mpya kila siku asubuhi; uaminifu wako ni mkuu. —Maombolezo 3:22-23

## MUNGU HUSIKIA MAOMBI

Maskini huyu aliita, BWANA akasikia, akamwokoa na taabu zake zote. —Zaburi 34:6

## MUNGU NI NGOME YETU

BWANA atakuwa ngome kwake aliyeonewa, naam, ngome kwa nyakati za shida. —Zaburi 9:9

## MUNGU HATAKUACHA

Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana BWANA, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha . . . Naye BWANA, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike. —Kumbukumbu 31:6, 8

## MUNGU HUTUPATIA AMANI

Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga. —Yohana 14:27

## MUNGU ATAKUONGOZA

Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako. —Mithali 3:5-6

## MUNGU HUTUFARIJI

Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu. —2 Wakorintho 1:3-4

## MUNGU HUTUPATIA PUMZIKO

Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. —Mathayo 11:28

# Wakati Wa Shida

## MUNGU ATATUPATIA NGUVU MPYA

Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo. Hata vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka; bali wao wamngojeao BWANA watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia. —Isaya 40:29-31

## MUNGU ATAKUTANA NA MAHITAJI YETU

Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu. —Wafilipi 4:19

## MUNGU ATATUONYESHA NJIA YA KUTOKEA

Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili. —1 Wakorintho 10:13

## MUNGU ANA MAWAZO BORA KWA AJILI YAKO

Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho. —Yeremia 29:11

## MUNGU ATAKUPIGANIA

Musa akawaambia watu, msiogope, simameni tu, mkauone wokovu wa BWANA atakaowafanyia leo; kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele. BWANA atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya. —Kutoka 14:13-14

## MUNGU ATAKUSAIDIA

Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini? —Waebrania 13:6

## MUNGU NDIYE NGUVU ZAKO

Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu. —Wafilipi 4:13

## KUJARIBIWA KWA IMANI YAKO

Hata ingawa huenda mtu akawa na furaha kubwa kwa muda, wakati mwingine mambo hubadilika, na badala yake akapatwa na uzito wa moyo kutokana na majaribu tofauti tofauti ambayo yamemkumba: Ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, iwapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo (1 Petro 1:6-7).

Ikiwa tutatembea karibu naye Mungu, tutagundua kwamba hata tukiwa ndani ya majaribu na kupatwa na machungu moyoni, kuna chemichemi ya kutuletea furaha ambayo itakuwa ndani mwetu kabisa katika nafsi zetu. Kwa njia ya kutambua kwamba sisi ni wa Bwana, ya kwamba anatupenda, na kwamba Yeye ndiye Msaidizi wetu – ukweli huu utatuletea furaha yenye kuleta utamu maishani, hata wakati tukiwa tungali katika masaibu ya maisha haya. Wakati mwingine, hata ikiwa furaha hii itafunikwa kwa muda kidogo kutokana na tashwishi na

woga ulioko mioyoni mwetu, lakini tukiendelea kujificha chini ya mabawa zake na kumtumaini kwa mioyo yetu yote, kinubi cha furaha kitasikika ndani kabisa nafsini mwetu, hata ikiwa tutajipata katika dhoruba za kihisia. Walakini, itatubidi sisi tusikilize undani wa mioyo yetu kwa makini sana, ili kuweza kuisikia sauti hiyo nyororo ya wimbo wa furaha, ambayo itatoka ndani mwetu.

Basi wewe kuwa mwenye subira katika majaribu unayopitia; vumilia magumu kama askari; dumisha ngao ya imani; pigana vita bora. Wakati utakapofika nafsi yako itaimba wimbo wa ushindi, ambao utaandamana na kengele za furaha, na kutoa muziki mtamu ambao utaita watu wa Mungu kufurahi pamoja nawe ndani yake Bwana na Mwokozi wako.

—“Mazungumzo ya Ana kwa Ana”  
kimeandikwa na C.W. Naylor

## FUNGA MLANGO WA MOYO WAKO ILI USIINGIE SHAKA

“MIALI YA TUMAINI” KIMEANDIKWA NA D.O. TEASLEY

Kushuku Mungu na kushuku neno lake ni tabia ambayo inatokana na Shetani, na kwa kiwango ambacho tutaendelea kumshuku Mungu, ndivyo ambavyo nguvu za shaka zitaendelea kutawala maishani mwetu. Kuwa na shaka ni jambo ambalo huunda njia katikati mwa bongo zetu, kama ambavyo watu wanaweza kuunda njia ya kutembelea shambani kupitia kwa nyayo za miguu yao. Jambo hili linaweza kushindwa tu kupitia kwa juhudi zetu kwa kupigana nalo kwa mioyo yetu yote na kwa nguvu zake Mungu, ili kwamba tuweze kuvunja nguvu hizo za kushuku mambo ya Mungu. Hebu basi nirudie tena: tabia ya kushuku ni jambo ambalo huletwa na mazoea au tabia ya mtu, na ni jambo ambalo chanzo chake ni Shetani . . .

Huenda ikawa kushuku ambako ni kubaya sana ni kule sisi kushuku mambo yale ambayo Mungu ameshafanya nafsini mwetu. Wale waliojaa moyo wa kushuku huwa wakifanya maombi mengi, lakini imani yao huwa ni hafifu sana. Ikiwa Shetanai atafaulu kuweka shaka moyoni mwako kuhusu ujuzi ambao tayari ushaupitia maishani na kutingisha ujasiri wako, hapo basi yeye hupata mweke wa kuingia nafsini mwako, na mwanya huo kamwe hautaifungika kwa haraka, na utakuletea shida ambazo hazina mwisho. Mimi ninajua watu ambao hutilia shaka mambo ambayo washapitia katika Mungu, na wanakuwa na tabia ya kwenda kwa Mungu kuomba msamaha, lakini hata kabla ya wao kuinuka kutoka maombini, wanaanza tena kumtilia Mungu shaka. Roho iliyojaa shaka ya kumwamini Mungu na ile ya mtu kujihukumu mwenyewe ni roho ambazo huwa na uhusiano wa karibu, na mara nyingi roho hizi hufanya kazi kwa pamoja.

Kwa watu wengine kumshuku Mungu huja likawa ni jambo la kawaida maishani mwao, na kumtuhumu Mungu linakuwa ni jambo rahisi hata zaidi ya kumwamini. Kama watu kama hao wangechukulia roho wa shaka vile ambavyo wachuuzi huchukuliwa na watu, basi wao hawangapatwa na shida nyingi kiasi hicho. Hii ni kwa sababu watu (wengi) hufunga milango yao wanapomwona mchuuzi akiwakaribia, hata kama mchuuzi huyo atajitetea na kuomba kupewa nafasi ya kuonyesha uzuri wa bidhaa anazouza. Ukweli ni kwamba kama watu wangepungua shaka zao nje ya milango ya mioyo yao hata kama shaka hizo zinaendelea kuomba kufunguliwa, basi shaka hizo zingeacha kuwakaribia maishani mwao mara nyingi hivyo.

Pia tendo la kushuku ni kama mgeni—ikiwa wewe utamkaribisha mgeni na kumburudisha nyumbani mwako basi mgeni huyo ataendelea kudumu hapo hapo nyumbani mwako; lakini kama utampuuza mgeni huyo na badala ya kumburudisha ukamkemea, mgeni huyo hatadumu hapo nyumbani mwako kwa muda mrefu, na hatakutembelea mara nyingi hivyo. Wasiwasi na mateso ambayo watu wanapata kutokana na tabia zao za kumshuku Mungu ni mambo ambayo yajulikana vizuri kwa wale wenye shaka hizo, ndiposa mimi sina haja ya kusema mengi sana kuhusiana na jambo hilo. ■

## KUTAZAMA MAHALI AMBAPO JUA HUCHOMOZA

“SIRI YA MOYO ULIO NA WIMBO” KIMEANDIKWA NA C.W. NAYLOR

Ni vizuri zaidi mtu kutazama mahali ambako jua huchomoza. Hata wakati ambapo tuko gizani, tunaweza kutazama mashariki ambako jua huchomoza, huku tukiwa na hakikisho kwamba punde si punde kutakucha. Tukiwa na imani kwamba tutapata marafiki wengine, hata ikiwa wale wa mbeleni wametuaacha. Kwamba kutachipuka tumaini jipya, hata ikiwa tumaini la mwanzoni limeambulia patupu. Kwamba kutakuwa na nafasi mpya zitakazoimbuka, hata ingawa za mbeleni zimedidimia. Hebu basi tufanye uamuzi kwamba tutaacha kutazama machweo ya jua, na badala yake tutazama mahali ambapo tunatarajia kupata mwangaza mpya; mahali ambako mwangaza mpya uliojaa utukufu utatungazia upya.

Lakini kutazama kule ambako jua huchomoza ni jambo ambalo mtu hujifunza. Jambo la kawaida kwa wengi wetu ni kuendelea kutazama mahali kule ambako jua limetua. Mkristo mwenye tumaini ndiye Mkristo mwenye furaha. Yeye hutazamia kupata mambo bora zaidi. Yeye hafi moyo. Kwa kweli mambo yote mazuri hayawezi kuwa yametupita milele. Mambo yanaweza kubadilishwa kwa mambo mengine. Mambo ambayo yatatendeka kwetu katika siku zijazo huenda yatategemea vile ambavyo tutayapokea, mtazamo ambao tuko nao kwa mambo hayo, na pia imani yetu ya kuyakaribisha mambo hayo. ■

## KUIMBA WAKATI WA SHIDA


“SIRI YA MOYO ULIO NA WIMBO” KIMEANDIKWA NA C.W. NAYLOR

Katika maisha haya watu hupitia mambo mengi magumu. Mambo kama hayo hayaepukiki. Magumu hayo huleta uchungu, majonzi, na hali ambazo humfanya mtu kufa moyo. Lakini haya ndio mambo ambayo Mungu hutumia ili kutujenga kwa mambo ya kiroho. Hivi ndivyo vifaa ambavyo mfinyanzi hutumia ili kutulainisha na kufanya tunyooke na tung’are. Ikiwa tutakuwa na mwelekeo kwamba hatuwezi kuwa na furaha hadi wakati tutakuwa katika hali ambayo hakuna kitu kinatusumbua maishani, furaha kama hiyo itakuwa ya muda mfupi sana. Furaha haipatikani kwa mtu kuishi maisha ya raha mutarehe na burudisho. Furaha ya kweli haitokani na ukosefu wa viziizi na mambo magumu maishani mwetu. Bali furaha kama hiyo hupatikana kwa sisi kuyashinda mambo hayo . . .

Tutakapokuwa katika matatizo tutapata wimbo mpya ambao ni tofauti na ule wa nyakati ambazo hakukuwa na matatizo. Ujasiri hauna budi kupatana na matumaini. Tunapokuwa na mwelekeo huo tunaweza kuimba nyimbo za ujasiri ambazo zimetokana na ujasiri wetu kwa Mungu. Tunaweza pia kuimba nyimbo za kumtumaini Mungu, nyimbo za kuondoa hofu zetu. Tunaweza kuimba nyimbo za matarajio, huku tukitazamia ushindi ambao uko mbele yetu, pamoja na taji ambalo tutapata tukimaliza safari hii yetu. Hata tutaweza kuimba nyimbo za furaha huku tukikumbuka rehema za Mungu ambazo zilituandama katika siku zetu za hapo mbeleni. ■

## IRUHUSU IMANI YAKO KUONGOZA HISIA ZAKO

“SIRI YA MOYO ULIO NA WIMBO” KIMEANDIKWA NA C.W. NAYLOR



Tunahitaji kuwa na imani na ujuzi wa wokovu ambo tumepitia kama Wakristo. Mimi nishawahi kukutana na watu wengi ambao walikuwa wamekufa moyo na ambao walikuwa na moyo wa kutomwamini Mungu. Nilipowauliza, “Shida

ni nini,” wengine walinijibu, “Sijihisi sawa.” Lakini nilipowauliza, “Ni kwa nini hujihisi sawa?” wengine wakanijibu, “Sijui ni kwa nini sijihisi sawa, lakini kwa kweli sijihisi sawa.”

Huenda ikawa ni kweli kwamba hujihisi sawa. Lakini hii ni kumaanisha nini? Hisia zako sio kipimo cha hali yako ya kiroho. Watu wengine hujihisi vibaya kimwili huku wakiwa hawana kitu chochote kilichoharibika mwilini mwao, au hata hawana kiungo chochote muhimu ambacho kinaugua mwilini mwao. Wakati huo huo kuna watu wengine ambao huwa wanajihisi sawa ilhali wanaugua ugonjwa ambao unaweza hata kuwaletea mauti. Ni vivyo hivyo kwa mambo ya kiroho. Kwa njia ya hisia zako huwezi kujua hali halisi ya uhusiano wako na Mungu. Hisia zako hazikukusudiwa kuwa ushahidi wa jinsi ulivyo kiroho. Basi tunahitaji kusimama wima kwa imani, na kujifunza kufanyisha kazi imani yetu, na pia kujifunza kuishi kwa imani. Hebu basi jihukumumu kwa njia ya haki. Usiruhusu hisia zako kuwa kipimo cha imani yako. Badala yake iruhusu imani yako kuongoza hisia zako. Kwa kawaida unapoamini kwa njia iliyo sawa basi utajihisi kwamba uko sawa; lakini wakati mwingi sisi huruhusu imani yetu kupimwa na hisia zetu, badala ya kwenenda kulingana na ukweli wa mambo ulivyo. Jinsi unavyohisi silo jambo muhimu sana. Hebu nikuulize tena, ukoje lakini? Jibu la swala hilo linastahili kuwa linalingana na imani yako, halistahili kamwe kutegemea jinsi unavyojihisi; na unapofanya uamuzi wa kupima imani yako kwa kipengele hicho basi hautaruhusu hisia zako kuwa dhibitisho la ukweli huo.

Kila siku tunahitaji kufanya mazoea ya kujenga imani yetu kwa kutumia mawe ya imani; badala ya kujenga kwa kutumia mawe ya shaka, woga, wasiwasi, na masumbufu ya kiakili. Kuna mawe mengi ya imani ambayo tunaweza kutumia kujenga. Na tunapojifunza kujenga kwa kutumia mawe hayo makubwa ya imani, basi tutaweza kujifunza Siri za Moyo Ulio na Wimbo—na kupata ujuzi wa kuwa na furaha, na pia ujuzi wa kufurahia safari yetu kama Wakristo, huku pia tukiwa na uhakika na siku zetu za usoni, na hata kuwa na uhakika wa maisha yetu ya sasa. ■

## KUTOKANA NA KUSHINDWA, TUNaweza KUPATA USHINDI MKUBWA ZAIDI

“SIRI YA MOYO ULIO NA WIMBO” KIMEANDIKWA NA C.W. NAYLOR



Je, ushawahi kujaribu jambo tena na tena lakini jambo hilo likawa lingali linakusumbua? Mtume Paulo alipitia mambo hayo yote. Kwa kweli unakumbuka ule “mwiba mwilini” ambao unatajwa kila mara. Mtume Paulo alijaribu kukabiliana na mwiba huo, lakini

Bwana hakumuondolea mwiba huo mchungu. Badala yake Yeye akamwambia, “Neema yangu yakutosha.”

Wakati mwingine sisi hujaribiwa kujitazama kama watu ambao tayari tumeshindwa. Kwa kweli sisi sote tushawahi kushindwa kuyafikia matumaini na malengo yetu ya kibinafsi. Lakini jambo moja ni wazi kabisa, kamwe hatutakuwa tumeshindwa kabisa ikiwa hatutasalimu amri na kuinua mikono yetu na kukubali kwamba tumeshindwa kabisa. Wakati mwingi ushindi mkuu zaidi hupatikana kutokana na kushindwa kwetu. Kile ambacho wakati mwingine huonekana kuwa ni kushindwa mwishowe huwa ni ushindi mkuu zaidi.

Kama hautaweza kufikia kilele cha matamanio yako basi fikia kile ambacho wewe unaweza kufikia, na usiwe wa kuonea jambo hilo aibu. Usiruhusu makosa au kukosa kutimbia utimilifu wote kukakuzuia kufanya kile ambacho unastahili kufanya.

Hebu basi fikia kiwango kile ambacho unaweza kufikia cha uwanaume au uwanawake wako, na uinue kichwa chako kutazama ulimwengu na hali zake (ana kwa ana), na utimize yote ambayo unaweza kufikia (kama mwanamke au mwanauume). Hebu basi ambia ulimwengu kwamba, “Nimekosa kufikia lengo langu, lakini sijashindwa kabisa. Nimekosa kutimiza malengo yangu, lakini ningali nitafaulu.”

Kuna mambo mengi ambayo inabidi watu kupitia—shida za kinyumbani, kuanguka kwa biashara, kulipa mikopo mikubwa, ulemavu wa kimwili, na mambo mengi kama hayo. Lakini hebu yatazame majina ya watu maarufu wa kihistoria na uone ni wangapi wao walikumbana na mambo kama hayo na wakaweza kuinuka juu ya mambo hayo, na wakaendelea kwa ujasiri hadi wakapata ushindi.

Kwa jambo lile maishani mwako ambalo kamwe haliwezi kusuluhishwa, wewe usikae kitako na kushikanisha mikono yako huku ukiomboleza, siku baada ya nyingine. Badala yake chunguza kile ambacho kinaweza fanyika katika hali ambayo imekupata. Bila shaka kutapatikana njia ya kupitia ambayo itakuongoza hadi uweze kufaulu na kupata ushindi. ■

“NAFSI YANGU YAMNGOJA MUNGU PEKE  
YAKE KWA KIMYA, WOKOVU WANGU  
HUTOKA KWAKE. YEYE TU NDIYE  
MWAMBA WANGU NA WOKOVU WANGU,  
NGOME YANGU, SITATIKISIKA SANA”  
ZABURI 62:1-2



JE, WAJUA?

“Mashujaa wa imani” ambao wanapatikana katika Agano la Kale walipata shida na matatizo mengi. Mitume wa Agano Jipya pia walipata upinzani mkubwa, na wote wakauawa kwa ajili ya imani yao isipokuwa mtume Yohana peke yake. Nao watakatifu ambao wanaonekana wamesimama mbele ya kiti cha enzi Mbinguni kwenye kitabu cha Ufunuo walikuwa wametoka “katika dhiki ile iliyo kuu” (Ufunuo 7:14). Ndiposa tunasema mateso na dhiki ni sehemu ya maisha ya Mkristo!



## MATESO HUMWEZESHA MTU KUWA NA HURUMA NA WATU WALE WENGINE

### “SIRI YA MOYO ULIO NA WIMBO” KIMEANDIKWA NA C.W. NAYLOR

*“Na ahimidiwe Mungu . . . atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu.”*

—2 Wakorintho 1:3-4

Mungu aliponiita katika kazi yake nilipitia masumbufu mengi ya moyoni. Masumbufu hayo yaliniumiza sana. Hata wakati mwingine karibu nikate tamaa. Lakini sasa mimi hutazama mambo hayo kama ambayo yaliniwezesha kuelewa moyo wa mwanadamu na kunifanya kuwa mtu mwenye huruma zaidi—na pia kunifanya kuweza kushiriki majonzi na mahitaji ya watu wale wengine, kwa kuniwezesha kuwaelewa, kuwapa faraja, na pia kuwasaidia; jambo ambalo nisingaliweza kufanya hapo mbeleni. Mateso



hayo ya mwanzoni yalifungua siri nyingi na kufanya maisha yangu na ya watu wengine kuwa yenye kina kikubwa zaidi. Hebu basi vumilia mambo kama hayo kwa subira, kwa maana kutokana na mateso unayopitia utapata kitu ambacho ni cha thamani zaidi hata kushinda dhahabu. Kama hujawahi sumbuka, basi wewe utakuwa wa faida kidogo sana kwa watu wale ambao wanapitia mambo masumbufu maishani mwao. Kwa kweli ahadi ambayo tumepata ni kwamba, “Kama tukistahimili tutamiliki pamoja naye.”

Abrahamu aliteseka wakati alipotoa sadaka kubwa zaidi maishani mwake (ya mwanawe Isaka), lakini mfano wake wa uaminifu umewahimiza maelfu ya watu. Naye Ayubu hakupitia tu maumivu ya kimwili bali pia maumivu makali ya ndani kabisa rohoni mwake; lakini ukweli ni kwamba, mateso hayo yalikuwa mweke wa Mungu kudhihirisha rehema na huruma zake. Je, ni mambo mangapi ambayo Ayubu alijifunza kwa kuvumilia siku hizo ambazo zilijaa giza, na ni masomo mangapi mazuri ambayo ulimwengu umejifunza kutokana na aliyopitia Ayubu! Basi kama tungeondoa kutoka kwa Biblia mambo yote ambayo yanaongea kuhusu mateso na matokeo yake, tungeinyang’anya Biblia mambo yote bora na yenye sifa kuu, na ambayo ndio yenye msaada mkubwa wa kusaidia na kuwahimiza wanadamu. Je, tungepoteza mangapi mazuri kama maandiko haya matakatifu yangukuwa yakisema tu kuhusu mambo ambayo humletea mtu furaha, amani na faraja! Kungekuwa vipi kama katika Biblia kuna hadithi tu za ushindi na watu kuweza kutimiza malengo ya maisha yao, huku ikikosa kutwambia lolote kuhusiana na barabara ngumu ambazo watu hao walipitia ili kupata ushindi huo. Ikiwa Bwana atatukemea, basi ni kwa ajili ya “faida yetu;” kama atatupiga kiboko, lengo lake ni kuyapatia maisha yetu utajiri mkubwa zaidi; hebu basi wewe kuwa na subira, vumilia kama mtu ambaye amemwona Bwana ambaye haonekani kwa macho. Tunahitaji kuwa na “subira katika dhiki,” na kunywa kikombo cha Gethsemane, kuvaa taji letu la miiba bila manunguniko, na kuvumilia msalaba wetu; kwa sababu tumeitwa ili kuteseka pamoja naye, na pia kutawala pamoja naye. ■

### Anwani

The Gospel Truth  
P. O. Box 2042  
Nixa, MO 65714  
USA

Email:  
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA